Jarida la
# RELI NA MATUKIO
SHIRIKA LA RELI TANZANIA
Toleo namba 32, Agosti 2023

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

## MSEMAJI MKUU WA SERIKALI AELEZEA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KIMKAKATI UKIWEMO WA SGR




Na Mwandishi wetu.

Msemaji Mkuu wa Serikali Ndugu Gerson Msigwa amekutana na waandishi wa habari kwenye mkutano uliofanyika katika jengo la stesheni ya SGR lililopo jijini Dar es Salaam na kuzungumzia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati ukiwemo mradi wa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa – SGR Agosti 26, 2023.

Ndugu Msigwa alisema Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania – TRC inaendelea na utekelezaji wa mradi huo wa SGR kwa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza una takribani

Inaendelea Uk. 2

## FIDIA ZA MRADI WA SGR ZAWANUFAISHA WANANCHI Uk. 3



# MSEMAJI MKUU WA SERIKALI AELEZEA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KIMKAKATI UKIWEMO WA SGR


Muonekano wa jengo la Stesheni ya SGR Bukwimba iliyopo Maswa mkoani Simiyu

Inatoka Uk. 01

kilometa 1219 na awamu ya pili kutoka Tabora hadi kigoma ni kilometa 506.

Awamu ya kwanza na ya pili ya ujenzi wa SGR nchini zinaifanya Tanzania kuwa nchi inayojenga mtandao mrefu zaidi wa reli ya kisasa barani Afrika (zaidi ya KM 2100), huku ikiwa miongoni mwa nchi chache za Afrika zinazotumia nishati ya umeme na teknolojia ya kisasa zaidi ya uendeshaji wa reli duniani (ERTMS Level ii)" alisema Ndugu Msigwa.

Aidha, Ndugu Msigwa alisema kuwa awamu ya pili ya ujenzi wa SGR kipande cha kutoka Tabora – Kigoma mkandarasi anaendelea na kazi za awali za maandalizi ikiwemo ukusanyaji wa vifaa na ujenzi wa kambi za ujenzi hali kadhalika zoezi la utwaaji wa ardhi na ulipaji fidia kwaajili ya ujenzi wa kambi zote tatu za Urambo, Nguruka na Uvinza limekamilika.

Vilevile, Ndugu Msigwa alieleza kuwa kupitia mkataba wa ununuzi wa mabehewa 30 na vichwa 2 vya treni kutoka kampuni ya Leuckemeire ya nchini Ujerumani, tayari mabehewa 6 yamekwishawasili nchini, mabehewa 24 yaliyobaki na vichwa 2 vinaendelea kukarabatiwa nchini Ujerumani.

"Serikali imenunua aina tofauti za mabehewa 1,430 ya mizigo kwa ajili ya reli ya kisasa ambayo yanaendelea kutengenezwa na kampuni ya CRRC ya nchini China pia utengenezaji wa mabehewa 59 ya abiria kutoka kampuni ya SSRST ya Korea ya Kusini, unaendela vizuri ambapo mabehewa 14 kati ya hayo yameshaingia nchini na mabehewa 45 yanaendelea kutengenezwa nchini Korea" alieleza Ndugu Msigwa.

Hata hivyo Ndugu Msigwa alifafanua kuwa utengenezaji wa vichwa 17 vya treni ya umeme na seti 10 za treni za kisasa EMU kutoka kampuni ya Hyundai Rotem ya Korea ya Kusini, unaendelea vyema na serikali inaendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kazi hiyo inakwenda kulingana na makubaliano.

"Kati ya vifaa vya uendeshaji tulivyokua tukitarajia kupokea mwishoni mwa mwezi wa saba ambavyo ni vichwa viwili vyenye kutumia nishati ya umeme kutoka nchini Ujerumani bado havijakamilika kutokana na changamoto ya baadhi ya vifaa ambavyo ni vipuli vilivyoagizwa nchini jirani kutopatikana kwa muda uliopangwa na kupelekea kuchelewesha utayari wa matumizi ya vichwa hivyo" alisema Msigwa.

Thamani ya uwekezaji wa serikali katika mradi wa SGR mpaka sasa ni zaidi ya shilingi Trilioni 23 za Kitanzania ambapo awamu ya kwanza na ya pili ya ujenzi wa reli ya kisasa nchi, zitaifanya Tanzania kuwa nchi inayojenga mtandao mrefu zaidi wa reli ya kiwango cha kimataifa barani Afrika.

# FIDIA ZA MRADI WA SGR ZAWANUFAISHA WANANCHI



Zoezi la malipo ya fidia kwa wananchi waliotwaliwa maeneo yao kupisha mradi wa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR Mwanza - Isaka likiendelea katika kijiji cha Ligembe mkoani Shinyanga, Agosti 2023.

Inatoka Uk. 2

Fidia zinazolipwa na Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania – TRC kwa wananchi waliotwaliwa maeneo yao kupisha mradi wa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa – SGR kipande cha Mwanza - Isaka zaleta faida na kuboresha maisha ya wananchi wa mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Simiyu, Agosti 2023.

Wananchi wamebainisha suala hilo kupitia zoezi la malipo ya fidia linaloendelea katika vijiji zaidi ya 50 vya mikoa ya Mwanza, Simiyu na Shinyanga ambapo zaidi ya Shilingi Bilioni moja zinaendelea kulipwa kwa wananchi waliotwaliwa maeneo na mali zao kupisha mradi wa SGR.

Faida zilizobainishwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba bora za kisasa, kukuza na kuendeleza shughuli za kilimo, ufugaji na biashara ambazo zinategemewa kwa kiasi kikubwa na wakazi wa maeneo husika.

“Kupitia fidia wananchi wameweza kujenga nyumba za kisasa na kupelekea kuboresha maisha yao, vilevile uzalishaji kupitia shughuli za kilimo umeongezeka kwani wapo baadhi ya wananchi wamenunua mashamba, vifaa, na pembejeo za kilimo pia kwa upande wa biashara wananchi wameweza kupata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza mitaji yao” alisema Bwana Zakayo Pastory, mkazi wa kijiji cha Ligembe

Pamoja na faida kadhaa zilizoonekana kupitia zoezi la ulipaji wa fidia tangu kuanza kwa mradi, Viongozi na Wananchi wamekuwa wakitoa ushirikiano kutokana na kutambua umuhimu na faida za mradi pamoja na fidia zinazolipwa na Serikali ili kutekeleza mradi.

“Faida ni nyingi, hizi tunazoziona hivi sasa ni sehemu tu ya faida kwani tumeona miji na vijiji vikikua kwa kasi kutokana na utekelezaji wa mradi huu, kwa upande wetu sisi ambao maeneo yatu yametwaliwa tunaipongeza Serikali tumeanza kula matunda ya mradi. Ushahidi upo wa kutosha ni namna

gani fidia hizi zinatunufaisha kwa kujenga nyumba za kisasa na kuendeleza shughuli za kiuchumi” alisema mtendaji wa kijiji cha Liboja, Bwana Takesh Simon

Mradi wa SGR umetoa faida nyingi wakati wa ujenzi ikiwemo ongezeko la ajira kwa wazawa katika sekta na fani mbalimbali, uboreshaji wa huduma za kijamii ikihusisha ujenzi wa shule, vituo vya afya na ujenzi wa barabara katika maeneo yanayopitiwa na mradi. Baada ya mradi kukamilika itasaidi uokoaji wa muda kwa usafiri wa abiria na mizigo na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mradi wa SGR Mwanza – Isaka unaendelea vema chini ya Mandarasi kampuni ya CCECC ya China ambapo umefikia 38.83% hadi mwezi Julai 2023. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa tuta, vituo vya abiria, ujenzi wa madaraja na makalavati pamoja na uwekaji wa mataruma, reli na nguzo za umeme katika baadhi ya maeneo.

Shirika la Reli Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi limekuwa likiendesha mazoezi ya utwaaji ardhi tangu kuanza kwa mradi wa ujenzi wa SGR jijini Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Simiyu na Mwanza ili kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya ujenzi wa mradi bila kuathiri Maisha ya wananchi. Hatua za awali za zoezi la fidia ni pamoja na uthamini ambao hufanyika wazi kwa kutambua mali na maeneo yanayotwaliwa pamoja na kuwashirikisha wahusika wakati wa uthamini.



# WANAFUNZI WA CHUO CHA RELI TABORA WATEMBELEA MRADI WA SGR

**Na Mwandishi wetu.**

Wanafunzi 35 wa Chuo cha Teknolojia ya Reli Tabora - TIRTEC wanaosoma masomo ya usafirishaji, ujenzi na matengenezo ya reli na kozi mbalimbali kwa ngazi ya Stashahada na cheti wametembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha Kimataifa kipande cha kwanza Dar es Salaam - Morogoro kuanzia stesheni ya Dar es Salaam hadi Pugu Septemba 5, 2023.

Makamu mkuu wa Chuo mipango fedha na utawala Bw. Edward Chezari amesema lengo la wanafunzi hao ambao wapo kwenye mafunzo ya vitendo ni kutembelea mradi ili kujifunza mambo yanayohusu ujenzi na uendeshaji wa treni za SGR kwa kuona mifumo mbalimbali ya kitalaam itakavyokua inafanya kazi pindi safari zitakapoanza pamoja na kuona mabehewa yatakayobeba abiria yaliyowasili nchini zikiwemo behewa za ghorofa.

"Wanafunzi wameona mfumo mzima wa chumba cha kongozea treni (control room) kutoka Dar es salaam hadi Makutupora utakaofanya kazi kupitia watalaamu watakavyofanya kazi kwenye chumba hicho" ameongeza Chezari

Rais wa wa Serikali ya Wananfunzi Chuo cha Reli Tabora Bi. Herieth Nelson amesema wamejifunza vitu vingi kuhusu mradi wa reli ya kiwango cha kimataifa ikiwemo usafarishaji wa wa abiria, mizigo na wanyama utakavyokua hapa nchini sehemu ambazo SGR itapita.

"Kupitia ziara hii tumeweza kujua tofauti iliyopo kati ya reli ya MGR (reli ya zamani) ambayo ni reli inayotumia mafuta katika uendeshaji wa treni na inaweza kuchukua muda mrefu kwa msafiri kufika eneo analoenda ambapo tumeona SGR inatumia umeme, ni usafiri wa haraka zaidi msafiri anatumia muda mfupi katika safari" ameongeza Herieth.

Waziri wa Elimu wa Serikali ya Wanafunzi kutoka chuo cha Reli Tabora Bw. Robert Pyakula ameishukuru menejimenti ya TRC pamoja na uongozi wa chuo kwa kuwapa nafasi ya kutembelea mradi kwani kupitia ziara hiyo wamejifunza mambo mengi ya uendeshaji wa treni ya SGR na anapenda kuwakaribisha wanafunzi waliomaliza elimu za kidato cha nne na sita wajiunge na chuo cha reli Tabora pamoja na Morogoro ili waweze kupata taaluma inayohusu utaalamu wa masuala ya reli.

Chuo cha reli Tabora kinatoa kozi katika taaluma ya usafirishaji, ufundi wa mabehewa ya treni, ujenzi na matengenezo ya reli, ishara ya mawasiliano ya njia za umeme pia kuna chuo cha reli tawi la Morogoro kinachotoa elimu ya taaluma ya ufundi wa vichwa vya treni na udereva wa treni.



Makamu mkuu wa Chuo Cha Reli Tabora - TIRTEC, Mipango Fedha na utawala Bw. Edward Chezari akiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wa TIRTEC na wahandisi wa TRC mara baada ya kutembelea jengo la Stesheni ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR jijini Dar es Salaam, Septemba 2023.

# MAMBO MUHIMU KUHUSU USALAMA WA RELI

- Usisikilize simu ama kutumia visikiliza simu masikioni na kupiga picha ukikatiza relini.
- Usiegeshe gari karibu na reli au kuweka kitu kizito kwenye reli.
- Usifanye uharibifu wa mazingira katika maeneo ya reli na maeneo ya miradi kwa kuchoma moto, kutupa taka, au vitendo vyovyote vinavyoweza kuhatarisha mazingira katika maeneo ya reli.
- Wafugaji wavushe mifugo maeneo maalumu ya vivuko.

### HATUA ZA KUFUATA UNAPOVUKA MAKUTANO YA RELI NA BARABARA

- Unapoona alama ya kivuko cha reli, simamisha chombo chako cha usafiri angalau mita 5 kutoka ukingo wa reli.
- Angalia pande zote mbili za reli na kuhakikisha kuwa hamna treni au kiberenge kinavuka.
- Iwapo hamna treni/kiberenge, vuka kwa muda usiozidi sekunde tatu.
- Kama kivuko kitakuwa na mfanyakazi wa reli au askari wa usalama barabarani, fuata maelekezo utakayoelekezwa na afisa huyo.

### CHUKUA TAHADHARI UONAPO ALAMA HIZI
















### ALAMA MUHIMU KWA WATUMIAJI WA RELI




Mbele kuna Reli inakatisha



Onyo la Mapema kuonesha mbele kuna treni zinapita



Kuwa makini unaposhuka kutoka kwenye Treni



Usitembee juu ya reli



Kuwa makini unapokuwa sehemu ya kupandia Treni



Usipande Treni inapokuwa kwenye mwendo




Vusha mifugo katika maeneo salama



Usining'inie dirishani au kuegemea milango unapokuwa ndani ya Treni

### RAMANI YA MAELEKEZO YA MATUMIZI YA MAKUTANO YA RELI NA BARABARA



# MATUKIO KATIKA PICHA



Mhandisi kutoka TRC Bi. Elvira Dominic akiwaonesha wanafunzi wa Chuo cha Reli Tabora picha mbalimbali za maendeleo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR ndani ya jengo la Stesheni jijini Dar es Salaam, Septemba 2023.



Afisa Usafirishaji kutoka TRC Bwana Masha Twaha Yasin akiwaelezea wanafunzi wa Chuo cha Reli Tabora kuhusu uendeshaji wa treni za kisasa za SGR walipotembelea jengo la Stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam Septemba, 2023.



Zoezi la kuhamisha makaburi ili kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Tabora - Isaka likiendelea katika kijiji cha Kakola kilichopo manispaa ya Tabora mkoani Tabora, Septemba 2023



Afisa Jamii kutoka Shirika la Reli Tanzania Bi. Alma Mulokozi (aliyevaa kizibao) akiwaelezea wananchi wa mtaa wa Lubaga kuhusu taratibu za malipo ya fidia wakati wa zoezi la ulipaji fidia mkoani Shinyanga, Agosti 2023.



Wanahabari kutoka vyombo vya habari mbalimbali nchini wakifuatilia mada kutoka kwa Msemaji Mkuu wa Serikali Bwana Gerson Msigwa (hayupo pichani) wakati wa mkutano wa waandishi wa habari uliofanyika katika jengo la Stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Agosti 2023.



Mhasibu kutoka Shirika la Reli Tanzania - TRC Bwana Yusuph Mrisho akiendelea na zoezi la malipo ya fidia kwa wananchi waliotwaliwa maeneo yao kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Morogoro - Makutupora lililofanyika mkoani Dodoma, Agosti 2023.



Kazi ya ujenzi wa daraja la juu la waenda kwa miguu ikiendelea katika mradi wa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR Mwanza - Isaka eneo la Nyashimbi mkoani, Shinyanga, Septemba 2023.



Kazi ya ujenzi wa daraja ikiendelea katika mradi wa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR Mwanza - Isaka eneo la Seke mkoani Shinyanga, Septemba 2023.



Kazi ya ujenzi wa daraja refu la kilomita 1.4 linalokatiza katikati ya jiji la Mwanza ikiendelea.



Kazi ya kujaza udongo kwenye tuta la reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Mwanza - Isaka ikiendelea katika eneo la Isaka mkoani Shinyanga, Septemba 2023.



Jengo la Stesheni ya SGR ya Seke likiendelea na ujenzi katika kipande cha Mwanza - Isaka cha mradi wa SGR mkoani Simiyu

# TRC YAENDELEA NA ZOEZI LA FIDIA MKOANI TABORA



Maafisa wa Shirika la Reli Tanzania wakiwahudumia wananchi wa kijiji cha Usongwahala wilaya ya Nzega mkoani Tabora wakati wa zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi waliotwaliwa maeneo yao kupisha mradi wa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa Tabora - Isaka, Agosti 2023.

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC linaendelea na zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi waliotwaliwa maeneo kupisha mradi wa reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR kipande cha nne Tabora - Isaka hivi karibuni Agosti, 2023.

Wananchi takribani arobaini na moja katika kijiji cha Usongwahala kilichopo wilaya ya Nzega mkoani Tabora wamekabidhiwa malipo yao na kupewa notisi ya siku kumi na nne ili waweze kumpisha mkandarasi kuendelea na ujenzi wa SGR.

Mthamini kutoka TRC Bw. Valentine Baraza alisema kuwa maeneo yaliyotwaliwa ni kwaajili ya ujenzi wa njia kuu ya reli ya SGR ambapo wananchi wote waliopitiwa na mradi walifanyiwa uthamini na kutoa taarifa zao kwa kushirikiana na mtendaji pamoja na mwenyekiti wa kijiji.

“Tunashirikiana na uongozi wa kijiji husika ili kuhakiki taarifa za mfidiwa sababu wao ndio wanaojua wananchi wa eneo lao kiusahihi zaidi” alisema Bw. Baraza.

Pia Mwenyekiti wa kijiji cha Usongwahala Bw. Kayagira Kajuba ametoa shukrani kwa serikali ya awamu ya sita ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwathamini wananchi kwa kuwapatia fidia kwa wakati na kusema kuwa kupitia malipo hayo mwanakijiji ataweza kujiendeleza katika kilimo na biashara mbalimbali.

“Watu watajenga nyumba za kisasa na biashara zitaongezeka kwa kasi zaidi” alisema Bw. Kajuba.

Mwananchi kutoka kijiji cha Usongwahala Bw. Kasepa Maganga alisema kuwa kupitia malipo ya fidia atajikwamua kiuchumi na kubadilisha maisha kwa kujenga nyumba ya kisasa na kuongeza mashamba.

Zoezi hilo la ulipaji fidia ni endelevu ambapo serikali kupitia TRC inahakikisha wananchi wote waliotwaliwa maeneo yao wanapatiwa stahiki zao kwa manufaa ya wananchi na Taifa kiujumla.

# IFAHAMU STESHENI YA SGR YA TANZANITE



**Na Mwandishi wetu**

Tanzania ni moja kati ya nchi zilizomo Afrika ya mashariki kati ya nchi saba ambazo nyinginezo ni nchi ya Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Congo na Sudani kusini. Nchi ya Tanzania imebarikiwa vitu mbalimbali vivutio vya madini ambayo hayapatikani kokote ulimwenguni nayo ni madini ya Tanzanite.

Tanzanite ni madini ambayo hayapatikani popote Duniani isipokuwa katika eneo la mji mdogo wa Mererani wilayani Simanjiro mkoani Manyara Kaskazini wa Tanzania, madini haya yana mchanganyiko wa rangi ya bluu na zambarau yaliyogundulika mwaka 1967 na kinachovutia zaidi kwenye madini haya ni uzuri wa rangi yake kubadilika kadri unavyoyatazama kupitia pande tofauti.

Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania – TRC linasimamia mradi mkubwa wa kimkakati wa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa wa SGR ambapo ndani ya ujenzi huo vimesanifiwa vitu mbalimbali ikiwemo njia kuu ya reli, majengo ya stesheni, madaraja ya juu na chini, njia za kwenye mahandaki na mifumo ya umeme.

Usanifu wa majengo ya stesheni za SGR umebuniwa katika miundo yenye maana tofauti zinazoonesha upekee unaopatikana katika nchi yetu ya Tanzania ikiwemo jengo la stesheni ya SGR lililopo jijini Dar es Salaam lenye muundo wa madini ya Tanzanite ambalo litakua kivutio tosha kwa Taifa.

Ndani ya Jengo hilo la stesheni ya Tanzanite kumesanifiwa mambo mbalimbali kuanzia nje ya jengo ambalo lipo mkabala na kituo cha mwendokasi kuna sehemu ya kupaki magari kwa watu wenye usafiri binafsi na usafiri wa umma. Jengo limeundwa kwa kuzingatia mahitaji ya watu tofauti kuingia na kupata huduma mbalimbali manunuzi na mapumziko.

Halikadhalika jengo hilo limewekewa miundombinu inyowezesha kutoa huduma za mpya (Standard Gauge Railway) na reli ya zamani (Meter Gauge Railway) kwa pamoja ambapo sehemu ya chini abiria wote wa reli ya zamani watakuwa wakipatiwa huduma kuanzia mapokezi, sehemu ya kukatia tiketi, sehemu zilizopo mashine za kukagua tiketi, sehemu za kusibiria treni na pakupandia treni kwaajili ya kuanza safari. Pia kuna sehemu maalumu ya mizigo ya abiria, kituo kidogo cha polisi, maduka na sehemu za maliwato.

Jengo la Tanzanite lina ghorofa takribani tatu, ghorofa ya kwanza ni maalumu kwaajili ya huduma za kibiashara ikiwemo benki na maduka ambavyo

# IFAHAMU STESHENI YA SGR YA TANZANITE




Inatoka Uk. 9

vitamuwezesha mtanzania na raia wa kigeni kufanya manunuzi bila ya kuwa msafiri na kwa kufanya hivyo ni dhahiri kuwa serikali kupitia TRC inabuni mbinu tofauti za kuongeza pato la Taifa.

Ghorofa ya pili ni sehemu maalumu ya kutoa huduma za reli yenye kiwango cha kimataifa ya – SGR ambapo abiria ataenda sehemu husika za kukatia tiketi ambapo kuna sehemu ya dirishani na kwenye mashine ambayo itamuwezesha abiria kukata tiketi kwa kutumia kadi aliyoiwekea fedha, kutumia kadi ya benki, kuingiza fedha taslimu ama fedha ambayo itamuwezesha kurudishiwa chenji yake papo hapo ambapo mashine hiyo ina sehemu kwaajili ya mteja kuingiza taarifa zake za mahali anapokwenda na daraja analotaka kukata na kuchukua tiketi, mashine hiyo imewekwa maandishi maalumu ya watu wenye uhitaji wa kuona katika kila hatua.

Baada ya kukaa Tiketi mteja ataelekea sehemu yenye mashine maalumu za kukagua tiketi ili mlango ufunguke na aweze kuelekea katika sehemu za kupumzika abiria ambapo kuna sehemu za abiria wa kawaida na abiria maalumu (VIP).

Sehemu ya VIP imeundwa kwa mandhari ya tofauti ambapo abiria atapatiwa huduma ikiwemo vitafunwa, kahawa, chai ama soda, pia kuna sehemu maalumu ya maliwato. Katika eneo hilo pia abiria anaweza toka nje na kuona jiji la Dar es Salaam kwa uzuri wake, baada ya mapumziko hayo abiria watapata matangazo punde tuu muda wa treni utakapofika na kuelekea eneo maalumu la kupandia treni.



Jengo la Tanzanite limewekwa maeneo mbalimbali zikiwemo ofisi za wafanyakazi, ofisi za uhamiaji ambapo raia wa kigeni watapita na kukaguliwa nyaraka zao, ofisi yenye mifumo ya kudhibiti uendeshaji wa treni iwapo njiani, mifumo mbalimbali ikiwemo kamera zinazoonesha jengo zima, lifti, skrini zinazoonesha ratiba ya treni, matangazo na mwenendo wa treni, mashine za kuskania tiketi na kukatia tiketi, ngazi zinazotumia umeme, alama maalumu kwaajili ya kupita watu wenye huitaji wakuona, mitambo ya kupimia mizigo.



Jengo la Tanzanite lina maeneo maalumu kwaajili ya mama kumpatia huduma na kumnyonyesha mtoto, pamoja na maliwato sehemu zote kuanzia sehemu ya chini hadi ghorofa ya tatu ambapo ni sehemu kwaajili ya huduma za kupata chakula na vinywaji kwa abiria na wananchi wote.

Jengo limejengwa kwa kutumia vioo imara vilivyozunguka jengo zima kwa umbo la madini hayo ya Tanzanite hivyo TRC ikishirikiana na wananchi wote ni vyema kuendelea kulinda miundombinu ya reli na kutumia usafiri wa reli ambao ni wa nafuu kwa abiria na kusafirisha mizigo kwa haraka.




**BODI YA WAHARIRI**
**MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk, MHARIRI MSAIDIZI/MSANIFU | Sami Omary**
**HABARI | Hemed Mohamed, Mariam Katunge MAKALA | Aziza Charles, Amina Juma, Athumani Iddy**
**PICHA | Musa Kadiko, Hassan Mbonde, Augustino Bulegea**